TANGAZO LA SERIKALI NA. 561 la tarehe 5/7/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16 (1))*

MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA YA MWAKA 2024

Jina
TS. Na.
284 2021

**1**. Sheria Ndogo hii zitajulikana kama Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Igunga ya Mwaka 2024, na itasomwa kwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ada na Ushuruya Halmashauri ya Wilaya ya Igunga ya Mwaka 2021 ambayo hapa inarejewa kama "Sheria Ndogo Kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 3

**2.** Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa kwenye kanuni ya 3 kwa kuifuta na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"Utozaji wa ada na ushuru

**3**.-(1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali kama ilivyoainishwa kwenye jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), ada au ushuru utakaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au kwa wakala ambaye atatoa stakakabadhi ya kielektroniki kama kielelezo cha kupokea malipo hayo."

Marekebisho ya kanuni ya 4

**3**. Kanuni Ndogo Kuu inarekebishwa kwenye kanuni ya 4 kwa kuifuta na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"Wajibu wa kulipa

**4**.-(1) Mtu yoyote anayetakiwa kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa

ada na ushuru

Sheria Ndogo hii, atatakiwa kulipa kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa.

(2) Haitakuwa utetezi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii mtu kudai kuwa amelipa ada au ushuru lakini hakupewa stakabadhi ya kielektroniki."

Marekebisho ya Aya ya 10

**4**. Kanuni Ndogo kuu inarekebishwa kwenye kanuni ya 10 (1) kwa-

(a) Kufuta nukta iliyoka mwishoni mwa aya (h) na badala yake kuweka neno "; na"; na

(b) Kuongeza, baada ya aya ndogo ya (h) kama ifuatavyo:

"(i) anafanya biashara bila kuwa na leseni ya biashara husika."

Marekebisho ya Jedwali la Kwanza

**5**. Kanuni Ndogo kuu inarekebishwa kwenye Jedwali la Kwanza-

(a) kwenye sehemu ya kwanza-

(i) kwa kufuta ada ya leseni ya crasher iliyopo aya XII.

(ii) Kwa kufuta ada za vibali vya kukusanya na kurundika mabaki ya bidhaa kwaajili ya kuchakata upya zilizopo aya XV na kuziandika upya kama ifuatavyo:

"XV. ADA ZA VIBALI VYA KUKUSANYA NA KURUNDIKA MABAKI YA BIDHAA KWAAJILI YA KUCHAKATA UPYA.

| Na. | Aina ya mabaki | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Chupa za Plastiki na mabaki mengine ya plastiki | 20,000/= kwa mwaka |
| 2 | Chuma chakavu | 50,000/=kwa mwaka |
| 3 | Mabaki ya kioo | 20,000/=kwa mwaka |
| 4 | Mabaki mengine ambayo hayajatajwa | 50,000/=kwa mwaka |

"

(b) kwenye Sehemu ya Pili-

(i) kwa kuifuta "2%" iliyoko kwenye aya I inayohusu Ushuru wa mazao ya kilimo, na badala yake kuandika "3%".

(ii) kwa kuifuta aya II na kuiandika upya

kama ifuatavyo:

"II. USHURU WA MADINI YA UJENZI

Kila aina ya chombo cha usafiri kinachobeba madini ya ujenzi kitalipia ushuru wa Shilingi 1,000/= kwa tani moja."

(iii) kwa kuifuta aya ya III na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"III. USHURU WA SHUGHULI ZA MADINI

| Namba | Aina ya Mazao | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Mchanga au mawe ya madini kwenye kiroba chenye ujazo wa kilo 50 unaosafirishwa nje ya eneo la uchimbaji, leseni ndani ya Halmashauri | 1,000/= kwa kila mfuko |
| 3 | Kila mwalo | 10,000/= kwa mwezi |
| 4 | Uuzaji wa marudio ya mchanga wa dhahabu<br>a) Uzito wa tani 1 - 9<br>b) Uzito wa tani 10-15 | 50,000/= kwa kila safari au tripu<br>100,000/= kwa kila safari au tripu |
| 5 | Elution Plant | 60,000/= kila column (tenki lenye Carbon) |
| 6 | Wenye leseni za madini wanapaswa kuwajibika kwa jamii (SCR) | 1% ya mapato yake kwa Mwaka |

"

(iv) kwa kuifuta aya VII na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"VII. USHURU WA STENDI

| Na. | Aina ya Chombo cha Usafiri | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mabasi makubwa | 2,000/=Kila inapoingia stendi |
| 2. | Mabasi ya kati (Coaster) | 1,500/=Kila inapoingia stendi |

| | | |
|---|---|---|
| 3. | Magari madogo Hiace na Noah | 1,500/=Kila inapoingia stendi |
| 4. | Teksi (Taxi),Pickup na kirikuu | 1,000/=Kila inapoingia stendi kushusha au kupakia abiria na mizigo |
| 5. | Piki piki na Bajaji | 500/=kila inapoingia stendi |
| 6. | Gari binafsi | 1,000/=kila inapoingia stendi |
| 7. | Chombo kingine ambacho hakikutajwa | 1,000/=Kila anapoingia stendi |
| 8. | Mtu yeyote anayeingia stendi kusindikizia au asiye na tiketi au kibali maalum cha kutumia stendi | 200/=Kila anapoingia stendi bila tiketi ya safari. |

”

(v) kwa kuifuta aya VIII na kuiandika upya ili isomeke kama ifuatavyo:

"VIII. USHURU WA TAKA

| Namba | Aina ya Chanzo cha Ushuru | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba ya kuishi kwa kila kaya yenye mtu 1 hadi 3 | 2,000/= kwa mwezi |
| 2. | Nyumba ya kuishi kwa kila kaya yenye watu 4 hadi 6 | 3,000/= kwa mwezi |
| 3. | Nyumba ya kuishi kwa kila kaya yenye watu 7 na kuendelea | 4,000/= kwa mwezi |
| 4. | Ofisi ya Taasisi au Asasi | 5,000/= kwa mwezi |
| 5. | Duka la Biashara ya Jumla | 10,000/= kwa mwezi |
| 6. | Washonaji wa nguo kwa cherehani | 1,000/= kwa mwezi |
| 7. | Mama au baba lishe | 3,000/= kwa mwezi |
| 8. | Duka lolote la rejareja, la bidhaa au huduma, lenye au linalostahili kuwa na leseni ya Biashara | 5,000/= kwa mwezi |
| 9. | Kioski au duka dogo | 3,000/= kwa mwezi |
| 10. | Saluni | 5,000/= kwa mwezi |
| 11. | Duka la kuuza nyama na au samaki | 10,000/= kwa mwezi |
| 12. | Duka la kuuza magari | 10,000/= kwa mwezi |
| 13. | Duka la Dawa za binadamu au wanyama au mimea | 5,000/= kwa mwezi |
| 14. | Ghala | 10,000/= kwa mwezi |
| 15. | Mgahawa | 5,000/= kwa mwezi |
| 16. | Baa | 10,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| | | kwa mwezi |
| 17. | Hoteli | 10,000/= kwa mwezi |
| 18. | Nyumba ya kulala wageni | 10,000/= kwa mwezi |
| 19. | Klabu ya usiku | 20,000/= kwa mwezi |
| 20. | Kumbi za sherehe | 20,000/= kwa mwezi |
| 21. | Zahanati (taka salama) | 5,000/= kwa mwezi |
| 22. | Kituo cha Afya (taka salama | 10,000/= kwa mwezi |
| 23. | Hospital (taka salama) | 15,000/= kwa mwezi |
| 24. | Hospital ya Rufaa (taka salama) | 20,000/= kwa mwezi |
| 25. | Kiwanda cha kuzalisha au kuuza mbao kwa taka ambazo sio mabaki ya mbao | 10,000/= kwa mwezi |
| 26. | Stoo ya Mkaa | 5,000/= kwa mwezi |
| 27. | Dobi | 2,000/= kwa mwezi |
| 28. | Wasindikaji wadogo wa mazao | 5,000/= kwa mwezi |
| 29. | Wasindikaji wakubwa wa mazao | 10,000/= kwa mwezi |
| 30. | Kiwanda kingine kidogo | 10,000/= kwa mwezi |
| 31. | Kiwanda kingine cha kati | 15,000/= kwa mwezi |
| 32. | Kiwanda kingine kikubwa | 20,000/= kwa mwezi |
| 33. | Kiwanda cha kukoboa mpunga, taka ambazo sio pumba | 10,000/= kwa mwezi |
| 34. | Shule binafsi ya kutwa | 10,000/= kwa mwezi |
| 35. | Shule binafsi ya Bweni | 20,000/= kwa mwezi |
| 36. | Kituo cha kuuza mafuta | 10,000/= kwa mwezi |
| 37. | Vituo vya kuoshea magari | 10,000/= kwa mwezi |
| 38. | Wauza matunda na mbogamboga | 1,000/= kwa mwezi |
| 39. | Maeneo ya taasisi na asasi za kiraia | 5,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| | | kwa mwezi |
| 40. | Wavundika ndizi na wenye vifungashio vya majani | 20,000/= kwa mwezi |
| 41. | Kituo cha michezo au mazoezi | 5,000/= kwa mwezi |
| 42. | Kilabu ya pombe ya asili | 15,000/= kwa mwezi |
| 43. | Karakana (Gereji) | 10,000/= kwa mwezi |
| 44. | Fundi viatu | 1,000/= kwa mwezi |
| 45. | Kituo cha mafuta | 10,000/= kwa mwezi |
| 46. | Kituo cha kubeti | 10,000/= kwa mwezi |
| 47. | Kituo cha kulelea watoto na wenye mahitaji maalum | Hakuna ushuru |
| 48. | Chanzo kingine ambacho hakikutajwa | 3,000/= kwa mwezi |
| 49. | Maeneo ya Magulio na Minada | 500/= kwa wiki |
| 50. | Grocery | 5,000/= kwa mwezi |
| 51. | Ofisi ya fundi Seremala isipokuwa mabaki ya mbao | 3,000/= kwa mwezi |

”

(vi) kwa kuifuta aya XIV na kuiandika upya kama ifuatavyo:

“XIV. USHURU WA ZANA ZA KILIMO ZINZOTUMIKZ KIBIASHARA

| Namba | Aina ya Zana na Matumizi | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Power tiller zinazofanya biashara kusomba mazao na mizigo mingine | 3,000/ =kwa safari |
| 2. | Mitambo ya kuvuna mazao(Combine harvestor) inayofanya kazi kibiashara | 500,000/= kwa msimu wa mavuno |

| | | |
|---|---|---|
| 3. | Trekta zinazofanya kazi kibiashara | 100,000/= kwa mwaka. |

”

(vii) kwa kuongeza baada ya aya XIV kama ifuatavyo:

"XV. USHURU WA MTAMBO WA KUSAGA MAWE YA MABAKI YA MADINI (KARASHA)

Ushuru wa mtambo wa kusaga mawe ya mabaki ya madini Karasha utakuwa Shilingi elfu kumi tu kwa mwezi.

"XVI USHURU WA KUSAFIRISHA NGOZI.

| Namba | Aina ya Mfugo | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) kwa kilo 1 |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 100/= |
| 2. | Punda | 100/= |
| 3. | Mbuzi | 50/= |
| 4. | Kondoo | 50/= |
| 5. | Nguruwe | 50/= |

XVII. USHURU WA MAEGESHO

**A) Ushuru wa maegesho wa maeneo maalumu ndani ya Halmashauri**

| **Namba** | **Aina ya Chombo cha Usafiri** | **Kiwango cha Ushuru (Shilingi)** |
|---|---|---|
| 1. | Magari makubwa ya mizigo (lori tani 7 na kuendelea | 3,000/= kwa siku |
| 2. | Magari makubwa ya mizigo (lori lenye uzito chini ya tani 7) | 2,000/= kwa siku |
| 3. | Mabasi ya kati (Coaster) | 2,000/= kwa siku |
| 4. | Magari madogo, Hiace na Noah | 2,000/= kwa siku |
| 5. | Teksi (Taxi) | 1,000/= kwa siku |
| 6. | Pikipiki na Bajaji | 500/= kwa siku |
| 7. | Gari binafsi | 1,000/= kwa siku |
| 8. | Chombo kingine ambacho hakikutajwa | 1,000/= kwa siku |

**B) Ushuru wa Maegesho ya magari kwa muda**

| **Namba** | **Aina ya Chombo cha Usafiri** | **Kiwango cha Ushuru (Shilingi)** |
|---|---|---|
| 1. | Gari yoyote ya mzigo | 1,000/= baada ya dakika tano |
| 2. | Mabasi ya kati(Coaster) | 500/= baada ya dakika tano |
| 3. | Magari madogo Hiace na Noah | 500/= baada ya dakika tano |
| 4. | Teksi(Taxi) | 500/= baada ya dakika tano |
| 5. | Pikipiki na Bajaji | 500/= baada ya dakika tano |
| 6. | Gari binafsi | 500/= baada ya dakika tano |
| 7. | Chombo kingine ambacho hakikutajwa | 500/= baada ya dakika tano |

”

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Igunga imegongwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa katika Mkutano wa baraza la Madiwani la Halmashauri ya wilaya ya Igunga uliofanyika tarehe 11 mwezi Agosti Mwaka 2023 na kushuhudiwa lakiri hiyo ikigongwa mbele ya:-

SELWA ABDALLA HAMID
*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri*
*Halmashauri ya Wilaya ya Igunga*

LUCAS MOGA BUGOTA
*Mwenyekiti wa Halmashauri,*
*Halmashauri ya Wilaya ya Igunga*

NAKUBALI

L.S

Dodoma
13 Mei, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais- Tamisemi*